




PreK 4 ME, Uhusiano wa Familia
SOMO LA 3: UPEPO NA MAJI

Muhtasari wa Somo la 3: Upepo na Maji


Tunapoanza Somo la 3, tunaendelea kufanya mazoezi na kukuza stadi za kijamii ambazo tumekuwa tukijifunza mwaka huu. Tunaanza masomo mapya kulingana na sayansi, ambayo inajumuisha kusoma hali ya hewa na jinsi inavyoweza kuwaathiri watu na wanyama. Tutafanya utabiri na kuchunguza dhana za sayansi kwa njia nyingi tofauti! Tunaendelea kujifunza kuhusu maneno yenye urari, sauti za herufi na dhana za kuhesabu darasani kwa mazoezi na michezo. Somo hili linatamatishwa kwa "Onyesho la Kujifunza" ili kuwapa wanafunzi wetu muda wa kutafakari kuhusu kujifunza kwao wakati wa Somo letu la Upepo na Maji. Soma zaidi!

VITABU VYA SPOTLIGHT vya Somo la 3




Gilberto and the Wind

Cha: Mare Hall



Rabbits and Raindrops

Cha: Jim




The Snow Day

Cha: Ezra Jack Keats

Thunder cake

Cha: Patricia Polacco



Picha zimepakuliwa amazon.com

Vitabu vingine mwezi huu ni pamoja...

- Time for Bed* cha Mem Fox
- A Hat for Minerva* cha Louise
- Living Things Need Water* cha Janet Morgan Stoeke
- Swimmy* cha Bobbie Kalman
- Swimmy* cha Leo Lionni

Nyimbo, Herufi na Michezo ya Lugha

Huu ni wimbo wa urari na kuhesabu ambao tunajifunza darasani—ujaribu mchezo huu ukiwa na mtoto wako na akuonyeshe jinsi anavyohesabu vidole vyake!

Vidole Kumi Vidogo

Nina vidole kumi vidogo, na vyote ni vyangu (inua vidole hewani)

Ninaweza kuviagiza vifanye mambo. Ugependa kuona?

Ninaweza kuvikunja kabisa, au kuvikunjua kabisa,

Kuviweka pamoja, Au kuvificha vyote.

Ninaweza kuvifanya viruke juu sana,

Ninaweza kuvifanya viruke juu kidogo,

Ninaweza kuvikunja pole pole, na kuvishikilia vyote hapo.



Picha imetolewa Pixabay

Angalia sehemu inayofuata uone mazoezi ya nyumbani



Wezesha Masomo ya Nyumbani Kupitia Mazoezi haya ya Ziada

Viwango vya Sayansi, Mbinu za Kujifunza, Hisabati na Lugha na Kusoma

Kuzama au Kuelea

Hili ni zoezi tunalofanyia darasani na unaweza kulifanyia nyumbani. Msaidie mtoto wako kukusanya karibu vifaa 10 na beseni ndogo ya maji. Mwambie mtoto wako avihesabu, akionyesha kila kitu wakati wa kuhesabu. Muulize mtoto wako maswali kuhusu ikiwa kila kifaa kitazama, au kuelea akikiweka ndani ya maji. Muulize aeleze utabiri wake. Unaweza pia kumwambia aorodheshe ni kitu gani kitazama au kuelea kisha umuulize kwa nini anafikiria kifaa hicho kilizama au kuelea.

Viwango vya Sayansi, Mwendo na Kusoma

Unda Chati ya Hali ya Hewa

Kwa kutumia chati iliyo hapa chini, mwambie mtoto wako achore aina za hali ya hewa. Msaidie kuweka lebo kila mchoro kwa neno la hali ya hewa.

Jadili kile mtoto wako anachoona akiangalia nje ya mlango au dirisha kila asubuhi, na ulinganishe hali ya hewa ya siku na picha aliyochora ya hali ya hewa. Jadili kuhusu mawingu, joto, mvua au theluji!


Viwango vya Sanaa, Sayansi, Mwendo na Mbinu za Kusoma

Sanamu za Mawingu

Ukitumia mojawapo ya viungo viwili vilivyo hapa chini, kulingana na viungo ulivyo navyo, wewe na mtoto wako mnaweza kutengeneza sanamu zinazofanana na mawingu!

1. Unga wa Wingu: Vikombe 2 vya unga na 1/4 ya Kikombe cha mafuta (mboga, mizeituni, mafuta ya mtoto– vyote hutumika!) Changanya na uanze kuunda sanamu!
2. Rangi ya wingu: changanya pole pole kikombe 1 cha povu la kinyozi na 1/3 ya Kikombe cha gundi ya nyeupe. Rangi hii yenye povu hukauka ikifanana na mawingu!

Image from brigidsdailylessonlog.blogspot.com



Ushauri kwa Familia na Wazazi: Miili yenye Afya

Kuna njia nyingi za kufundisha watoto kuhusu kudumisha afya njema. Hivi hapa ni vidokezo vichache kutoka CDC:

- ⇒ Kula chakula ukiwa na mtoto wako kila inapowezezana. Mwonyeshe mtoto wako kuwa unafurahia kula matunda, mboga na nafaka wakati wa mlo na vitafunio. Mtoto wako anapaswa kula na kunywa kiasi kidogo tu cha chakula na vinywaji ambavyo vimeongezwa sukari, mafuta au chumvi.
- ⇒ Hakikisha chumba cha kulala cha mtoto wako hakina televisheni. Weka masharti ya muda wa kutumia vifaa vya burudani yasiyosizidi saa 1 kwa siku, ukihakikisha wanatazama vipindi bora nyumbani, shuleni au vituo vya malezi, na uandae ratiba ya matumizi ya vifaa vya burudani ya familia yako.
- ⇒ Mpe mtoto wako vifaa vya kucheza vinavyolingana na umri wake, kama mipira na vifaa vya plastiki, lakini mruhusu mtoto wake anayekaribia kujiunga na shule ajichagulie vifaa vya kucheza. Hatua hii humrahisishia mwendo na kufanya mazoezi.
- ⇒ Hakikisha mtoto wako analala kwa kipindi kinachopendekezwa kila usiku: watoto wanaokaribia kujiunga na shule wa miaka 3-5, wape saa 10-13 kila saa 24 (pamoja na kulala mchana)